MAISHA YA MKRISTO. **SOMO LA 4.**

Itikio kwa Biblia na haja ya ubatizo.

TAFADHALI BIBLIA YAKO IWE IMEFUNGULIWA NA UJARIBU KUANGALIA VIFUNGU VYOTE REJEA.

Wakati mtengenezaji wa vifaa vya nyumbani anaweka tangazo katika gazeti, watu ndiyo husoma na kuitikia kwa kununua bidhaa hizo. Wakati Mungu katika uumbaji wake aliyapa maua harufu na rangi za kung'ara ilikusudiwa hivyo ili kuvutia wadudu ambao wangesambaza poleni kutoka ua hadi ua jingine na hivyo kuruhusu mmea kutengeneza mbegu. Kwa njia kama hii Mungu alipotoa neno lake ambalo leo tunaita Biblia, alifanya hivyo ili wanaume na wanawake waweze kusoma na kuongozwa kwa kutii wito uliomo.

Katika kila hali, sababu zitolewazo kwa lolote linalofanywa ni "Uhai". Mwenye kiwanda anataka Kampuni yake idumu na iendelee kupata faida, vichaka na maua sharti vizae mbegu ili jinsia yake iendelee kuishi, na Mungu katika neno lake Biblia ameahidi maisha ya milele kwa wote wanaofikia ujumbe wake.

Watu hununua bidhaa katika maduka huweza kufanya hivyo kwa sababu inaonekana kuwa ni vema kufanya hivyo katika wakati huo. Ndege na wadudu wanaonekana kutojali huduma wanayoitoa kwa mimea na maua ili mradi wao watapata maji maji ya maua (utomvu) wa maua. Hata hivyo ni jambo tofauti unaposoma Biblia na kuongozwa kutii yaliyomo. Je unatakiwa ufanye nini?

Yesu alisimulia mfano wa mpanzi akipanda mbegu kuelezea swali hili hili na ukifungua Biblia yako katika Luka sura ya 8 mistari ya 4 hadi 8 unaweza kusoma mwenyewe. Iwapo utaona maneno ya Yesu ni magumu kuyaelewa usijali kwani hata wanafunzi wake Yesu hawakuweza vile vile kuelewa na katika mstari wa 9 tunaambiwa kwamba waliomba ufafanuzi. "Mbegu ni neno la Mungu" Yesu alisema inaonekana na kusikiwa na watu wa aina mbalimbali. Wako wale wasioafiki wako sawa na mbegu iangukayo kandokando ya njia wengine wanaonekana kujali kidogo na mara wanaisogeza pembeni Biblia na kuendelea kufanya mambo mengine wanayofikiria ni muhimu. Aidha kuna watu wanaoafiki kwa furaha na kukubari kwa dhati kuwa wafuasi wa yesu lakini tabu na usumbufu wa maisha yao yanawafanya wawe na muda mfupi wakusoma, hupata muda wa kusali, hatimaye kukata tamaa kabisa . Hawa ndio watu wanaokatisha mbegu inayoangukia katika miiba. Mbegu inayoangukia katika ardhi nzuri inakuwa na kuzaa matunda. Hakika watu hawa watakuwa wanafunzi. Kwao Biblia ni kitabu

muhimu sana katika misha yao. Wanapokuwa katika matatizowazo lao la kwanza ni kusali, kwamba msaada wa mwongozo hata kama watakumbana na upinzani hawamwachi Yesu awe njia ya mwamba wao. Hii ndio maana ya kumfuta yesu kwa dhati. Haiji kwa kujifunza injili tu, ni uthibitisho wa ndani ambayo ni ya utu binafsi. Uhusiano unaendelea kati yako na muumini yesu na mungu baba yake.

Sasa angali Injili ya Yohana sura ya 14 mstari wa 23 yesu alikuwa akisema kwa marafiki wake wa karibu mutume. Yuda Iskarioti. Mtu ambaaye alimsaliti kwa askari wa kuhani mkuu alikuwa ameondoka kutoka katika chumba. Hii ni ahadi maalumu ya pekee na inahusu waumini wa nyakati zote kuanzia wakati huo katika Yohana sura ya 15 mistari ya 1 hadi 9 tunaona Yesu akitumia neno lingine la picha ambayo safari hii alijisema yeye kuwa ni mzabibu, Matawi yalikuwa na yanaendelea kuwa wanafunzi wake na katika mstari wa 8 tunapelekwa kwenye wazo la kuzaa matunda. Zaidi ya hayo tunaambiwa wazi kuwa tunapofikili kikamilifu wito wa Yesu na kutoa maisha yetu kwa huduma yake Mungu anatukuzwa.

Kwa mifano mingi katika Agano Jipya ya watu kukubali wito wa Injili ya Yesu; kuanzia kwa Zakaria akikwea mti ili kumwona Yesu, Luka sura ya 19 mistari ya 2 hadi 10, kwa mwanamke mzinzi ambaye alileta sanduku la manukato ya thamani kubwa ili kumpaka Yesu miguu yake, Luka sura ya 7 mistari ya 37 hadi 50. Katika kila kisa inaonyesha hamu ya kukubali wito wa ridhaa ya kutaka kujitolea bidhaa au fedha kuthibitisha hiyo ridhaa. Yesu hakuomba vitu kama hivyo lakini hii ilikuwa ni hatua ya kwanza ya mtu binafsi ufanyike kuwa mwanafunzi.

Siyo watawala wote wa Mayahudi ambao hawakumtaka Yesu. Wakati wa kusulubiwa kwake, wawili kati yao Nikodemu na Josefu walimwendea Pilato kuomba idhini ya kupewa mwili ili uzikwe kwa heshima - Injili ya Yohana sura ya 19 mistari ya 38 hadi 42. Kwa kufanya hivyo waliobainika wamo na baadaye wanateseka sana kwa sababu ya kuwa wafuasi wa Yesu. Mara nyingi Wanafunzi vilevile waliokabiliwa na tatizo gumu la kuamua kuacha mali na maisha ya raha na kukubali shida ili waweze kuwa wafuasi wa Yesu. Yesu alitoa ahadi kwa wafuasi wake alipozungumza na Petro juu ya suala hili- tazama Mathayo sura ya 19 mistari ya 27 hadi 29.

Kutokana na mifano hii ni wazi kwamba kuwa mwanafunzi wa Yesu ni jambo zito linalohitaji kufikiri sana. Sio jambo la kulikimbilia halafu baadae ukaanza kujuta. Huu utakuwa uamuzi utakaoweza kubadilisha maisha yako mpaka muda wa kufariki kwako au Yesu atakaporejea duniani kama Mfalme aghalabu kutegemea tukio litakalotangulia kwa hali iwayo yoyote ile uamuzi utakaowachukua utakufanya uendelee hatua ya mbele na hiyo itakuwa ubatizo.

Katika masomo yaliyopita, tumeonyesha umuhimu wa ubatizo, jinsi ilivyokuwa ni amri ya Yesu kwamba wote wanataka kumfuata sharti wafanye hivyo kwa ubatizo wa maji. Injili inatuambia kwamba Yohana Mbatizaji alikuja mbele ya Yesu akibatiza ubatizo wa toba kutoka katika dhambi. Yesu mwenyewe alionyesha mfano kwa kumwendea Yohana na hapa ndiyo mwanzo wa wanafunzi wote watakaomfuata tangu siku ile na kuendelea. Tendo la ubatizo tangu awali ilikuwa kuzamishwa katika maji. Mara Yesu alipokuwa akitoka ndani ya maji, Mungu alionyesha kupendezwa na kitendo cha mwanae kwa kutuma nguvu zake katika umbo la njiwa kutua juu yake. Mathayo aliandika juu ya hili katika sura ya 3 mistari ya 13 hadi 17. Angalia jinsi Mungu alivyozungumzia kuhusu kupendezwa na kumkubali Yesu kuwa mwanae katika ubatizo huu. Marko aliandika mojawapo ya maagizo ya mwisho ya Yesu kwa wanafunzi wake kabla ya kupaa mbinguni. Angalia sura ya 16 mistari ya 15 na 16. "Enendeni ulimwenguni mwote na mkahubiri Injili. Yule anayeamini na kubatizwa ataokoka.

Ukweli wa umuhimu wa ubatizo ulieleweka zaidi baada ya kifo cha Yesu. Waandishi kama Paulo na Petro, kwa nguvu za Roho Mtakatifu walianza kuonyesha kuwa ubatizo ni ishara ya kifo na ufufuko - Warumi sura ya 6 mistari ya 3 hadi 6. Kuna mambo mengi muhimu ya kujifunza kutoka maneno haya. Kitendo cha waumini kuzamishwa majini kwa muda kinawakilisha kifo cha Yesu. Kuinuliwa kwa waumini kutoka katika maji kunawakilisha ufufuko wa Yesu. Kama vile Yesu alivyobadilishwa baada ya ufufuko wake nasi pia tunabadilishwa, sio kwa kuonekana, sio kwa huzuni, kuwa huru wa majaribu ya dhambi, lakini kwa haiba, sasa tukitembea katika upya wa maisha, dhambi zetu zikiwa zimesamehewa kwa sababu ya kujitolea kwa Yesu.

Paulo alitumia mfano wa utu wetu wa awali ukisulubiwa naa kuacha nyuma dhamira mpya ya kutupeleka mbele kumfuata Yesu, tukiwa na ongezeko la ushupavu na mafanikio. Kuna agizo moja muhimu ambalo liko katika mstari wa 6. Kwamba hivi sasa tusihudumie dhambi. Paulo anaendelea katika kifungu hiki kueleza alikuwa na maana gani katika usemi huu na kama unao muda, angalia mistari ya 14 hadi 23. Mabadiliko katika maisha yetu na jinsi tunavyokuwa sehemu ya kusudio la Mungu kuwa katika dunia hii ambayo imeonyeshwa katika Waraka kwa Wagalatia sura ya 3 mistari ya 26 hadi 29. Mfumo huu wa urithi wa Utukufu ambao utakuja juu ya nchi, ni matarajio yetu nyeti ambayo sasa wewe unayo nafasi ya kushiriki.

CBM Publishing, 32 Blenheim Rd, Far Cotton, Northampton NN4 8NW United Kingdom
PO Box 2950, Mbeya, Tanzania (East Africa)